

**KUANGALIA KULE KUTIMIA KWA
AHADI ZA MUNGU KATIKA SIKU ZETU**

Inategemea kile unachoangalia ni nini. Unaona nini unapoangalia? Kumbuka, unaweza ukamuona Yeye tu pale unapomuangalia kupitia Neno lake. Huwezi ukamuangalia Yeye kupitia kitabu cha mafundisho. Huwezi ukamuangalia Yeye kupitia kanuni za Imani. Utaona Miungu miwili au mitatu, na vitu vinginevyo vyote katika kanuni hizo za Imani. Lakini Muangalie Yeye kupitia Neno, na utaona kwamba Yeye ni Immanueli – Mungu aliyefanyika mwili miongoni mwetu. Alisema, “Mimi ni Mungu na zaidi ya Mimi, hapana mwingine. Yeye ni Mungu [1]

Yesu alisema mahali fulani, kwamba Neno ni mbegu (Luka 8:11). Na kila mbegu itazaa kwa jinsi yake (Mwanzo 1:12). Na sasa, kama wakristo, watoto wa Mungu, watoto wa ufalme wamekuwa mbegu ya Mungu, kwa hiyo lazima wawe ni Neno la Mungu, Neno la Mungu lililodhihirishwa katika wakati ambao wanaishi, kwa mbegu iliyo ahidiwa ya wakati huo (Matayo 13:37 – 39). Mungu alitoa Neno lake pale mwanzo, na kila wakati umekuwa na mbegu, kwa majira yake, ahadi zake.

Sasa, wakati Nuhu alipokuja katika mazingira yake, na yeye alikuwa ni mbegu ya Mungu, Neno la Mungu kwa wakati ule (Mwanzo 6:9).

Wakati Musa alipokuja, hangeweza kuja na ujumbe wa Nuhu; usingefanya kazi, kwa sababu yeye alikuwa mbegu ya Mungu ya wakati ule (kutoka 3:1).

Sasa wakati Kristo alipokuja, asingeweza kuja na wakati wa Nuru au wa Musa; ilikuwa ni wakati wake, kwa bikira kuchukua mimba na kuzaa mwana, na yeye angekuwa ni masihi (Isaya 7:14); (isaya 11:1-5). Sasa, tumeishi kupitia wakati wa Luther, wakat wa Wesley (wakati wa methodist), nyakati zote kwenda chini, na wakati wa Pentecoste, na kila wakati ulipewa ahadi ya Neno. Na watu wa wakati ule walidhihirisha Neno lililoahidiwa ambalo ni mbegu ya wakati ule, kutokana na Yesu alivyosema mahali hapa, Ni watoto wa ufalme”. Hiyo ni sawa. Udhihirisho wa Roho Mtakatifu akitenda kupitia watoto wake ambao ni mbegu za ufalme katika wakati ule [2].

Sasa, kile chote tulicho nacho leo ni kudhihirisha tabia zake. Mwanzo Yeye hakuwa hata ni Mungu, Mungu, tungemwita Yeye kuwa Yule wa milele. Hakuwa ni Mungu, kwa sababu Neno, neno la kiingereza, “Mungu” inamaanisha “Kitu kinacho abudiwa” na hakikuwepo chochote kumuabudu Yeye kwa hiyo yeye alikuwa Yule wa milele, lile chimbuko la chemchemi ya maarifa yote na chimbuko hili la chemchemi ya maarifa hakukuwa na chembechembe au chochote, hakukuwa na Nuru, nyota, mwezi wala chochote. Mungu, tunayemjua kama Mungu, Yule Roho mkuu ambaye ni wa

milele, kamwe hana mwanzo, kamwe hana mwisho. Alikuwa pale. Na ndani yake kulikuwa na sifa. Ilikuwa sifa ya kuwa Mungu, halafu sifa yake ya kuwa Baba, sifa ya kuwa Mwana, sifa ya kuwa Mwokozi, sifa ya kuwa Mponyaji. Sifa hizi zote zilikuwa ndani Yake. Na sasa, mambo haya ambayo yamejifunua tangu wakati huo ni sifa zake zikiwa zinadhihirishwa.

Ninachomaanisha, “sifa” ilikuwa ni mawazo yake. Na Neno ni mawazo yaliyodhihirishwa. Na sasa haya yalikuwa ni fikira zake. Na wakati aliposema, “kiwepo hiki”, na kikawepo” na pale sasa ilikuwa (Mwanzo 1:3). Na sasa, kumbuka, ninyi wakristo mlikuwa ni mawazo Yake kabla haijakuwepo dunia. Na ninyi ni udhibitisho wa mawazo Yake. Kabla hata haijakuwepo dunia, mlikuwa mko ndani ya Kristo, ndani ya Mungu kule mwanzoni (Waefeso 1: 3 – 6; 1Tim 1:9 – 10). Hilo linawafanya kuwa ni washirika wake. Na jambo lote ni Mungu mwenyewe, akijionyesha katika umbile lake la kushikwa ili kwamba aweze kuguswa, kuonekana, na kuthalika. Na hivyo ndivyo Mungu alivyo, jambo hilo lote.

Mungu ni mtafsiri wake Mwenyewe. Hahitaji mtu yeyote atafsiri kwa ajili Yake. Anafanya tafsiri yake Mwenyewe. Ni mtu nani anayeweza kumtafsiri Mungu? Mungu ni Mtafsiri Wake Mwenyewe.

Tunaona kwamba pale mwanzo Mungu alisema, “Na iwepo Nuru” na ikawepo Nuru, hiyo ndiyo tafsiri kwa hilo. Mungu aliposema chochote, na kilidhihirishwa, na hapo sasa huyu ni Mungu akitafsiri kwamba Neno lake ni kweli. Unaona? Wakati aliposema “iwepo Nuru”, hilo lilikuwa katika Mawazo Yake kabla haijakuwepo kitu kama Nuru. Wakati aliposema “Iwepo Nuru”. Nuru ilitokea angani; hiyo ilikuwa ni tafsiri ya (Mwanzo 1:3-5). Hakuna yeyote wa kutafsiri hilo, kwa maana Mungu alisema hivho na ikawa hivyo. Wakati Mungu anaponena na inadhahirishwa, hiyo ndiyo tafsiri ya Neno lake. Kwa nini watu hawawezi kuliona hilo? Kwa nini watu hawalion hilo?

Wakati Mungu anapoweka ahadi na Mungu anasema pale mwanzoni katika Mwanzo, Aliligawanya Neno lake kwa kila wakati kwa kadiri lilivyokuwa linashuka kutoka mwanzo mpaka mwisho. Na ukifuatia chini katika hizi nyakati za kanisa, dunia imesichanganya zote wa sababu ya mapokeo na kadhalika; Mungu hutuma manabii katika matukio, kuanzia tangu agano la kale mpaka jipya. Na Neno la Mungu linakuja kwa Manabii (Amos 3:7; Matayo 23:37). Na hilo linafanyaje? Inadhihirisha Neno la Mungu. Udhihirisho wa Mungu, unaosema hilo kama ni sahihi au siyo sahihi. Hakuna mtu ambaye anapaswa kulitafsiri hilo; Neno linajitafsiri lenyewe. Mungu ameliahidi na hilo limetokea.

Kuna gaida gani ya kusema chochote juu ya hilo? Mtu nani mwenye dhambi ambaye atajaribu kusema (wakati Mungu ametoa ahadi za Mungu anaitimiza) kwamba tafsiri hiyo sawa? Huyu ni Mungu mwenyewe alifanya tafsiri, tafsiri yake mwenyewe. Yeye hahitaji mtu yeyote amtafsirie Yeye, Yeye anatafsiri Mwenyewe kwa kulidhihirisha lile aliloahidi kwamba atalifanya.

Oh, kama tu kanisa lingaliona hilo na kuona ahadi zilitotolewa kwa kila wakati! Nyakati nyinginezo zote, Mungu ametuma katika matukio (Hata ukifuatilia nyakati zote saba za kanisa) na amedhihirisha kila kitu alichohidi kufanya. Kila kitu hakuna kitu alichocha kukifanya. Hakika! Kile alichosema atafanya, hicho alikifanya [3]

Mungu wa ulimwengu leo, mtu anayeabudiwa leo katika ulimwengu/dunia ni shetnai, na watu hajui kwamba wanamwabudu shetani (2Wathesalonike 2:3-4). Lakini ni shetani aliingiza na kuja kama kanisa. Wanamuabudu shetani wakifiri wanamuabudu Mungu kupitia kanisa, lakini ni njia ambayo shetani amelifanya hilo (Marko 7:7 – 13).

Oh, unasema, “Lakini ngoja dakika; tunahubiri Neno” Anglaia nyuma pale katika somo langu. Shetani ndiye aliyemhubiria Hawa Neno kwa mara ya kwanza. “Mungu amesema” (Mwanzo 3: 1 – 5). Ni kule kupotosha kidogo sehemu ya mandiko inayohusika na ule wakati. Atakuacha ujue yale yote aliyoyafanya Yesu kwamba ni makamilifu. Atakuacha ujue kwamba yale yote aliyoyafanya Musa yalikuwa sawa swa. Lakini ukichukua ahadi alizozitoa kwa siku ya leo; hapo sasa hiyo ilihusu wakati mwingine. Hivyo ndivyo awezavyokufanya ili awapae watu waliani hilo kwa namna hiyo, na ni hilo tu. Kwa maana huwezi ukachukua Neno moja kutoka kwenye hilo au kuongeza Neno moja kwa hilo, lakini hivyo ndivyo anavyofanya.

Ule udanganyifu wa kanisa la leo unaona, mwana wa uharibifu, shetani, mwana wa uharibifu, shetani Hapo watu wanamuabudu shetani kupitia kanuni za imani, tungo za kidhehebu zilizofanywa na watu na kanuni za imani, ndizo zimewaleta watu kwenye udanganyifu mkubwa sana uliowahi kujulikana duniani. Haijalishi Neno la Mungu limeahidi nini kwa siku ya leo, lihubiriwe na lithitishwe, bado hawataliamini hilo. Hawataliani hilo.

Ni kwa nini? Tunashangaa ni kwa nini. Kwa nini ... kwa nini wasiliamini hilo, wakati Mungu alisema atafanya jambo fulani, na Yeye akalifanya; na bado wanageuza migongo yao, na kwenda mbali nalo? Kama vile tu Hawa lajua kile Mungu alisema, Mungu atafanya; Lakini aligeuza mgongo wake kumsikiliza (shetani) kile ambacho atasema. Kumbuka hilo, katika nyakati nyingine, imekuwa hivyo mara zote jambo lile lile. Kila wakati imekuwa kila mara shetani amejaribu kupotosha Neno kwao, kuwafanya waone wakati mwingine.

Sasa, alianza kwa udanganyifu wa kidini pale Edeni na ameendelea tangu wakati huo, sio kwa kuweka kundi la wakomunisti. Imekuwa ni udanganyifu wa kidini tangu pale mwanzoni edeni, na imekuwa hivyo tangu hapo.

Wakati wa Adamu ilikuwa ni udanganyifu. Wakati wa Nuhu, ilikuwa ni udanganyifu wa kidini [4]

Imegeukia kwenye Neno, angalia Neno limeahidi nini leo, angalia uone Nuru ya siku ya leo ni nini. Oh, kanisa, geukieni Neno, rudini kwenye Neno, washa swichi sahihi; achana na kuilinda taa ya umeme, taa ya kujitengenezea, iliyoundwa na watu. Geukia Neno lake na uone ahadi ya siku ya leo. Na uangalie hiyo ahadi inasemaje na uone vile inavyotambulishwa. Pale inapothibitishwa, hapo unajua uko kwenye Nuru au hapana. Angalia ahadi inasemaje.

Kwangu mimi, nataka kuona kile kilicho ahidiwa kwa siku ya leo. Natka kufahamu ile Nuru ya saa hii, ili nijue namna ya kutembea ndani yake. Nataka kujua ni wapi ninaishi, ni wakati gani tuko, tuko umbali wa njia kiasi gani?

Kama Paulo alivyosema, naweza kurudia kunukuu tena, “Nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele, nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu”, kwenye utambulisho mkamilifu, wakati muda utakapoishia ndani ya umilele wakati Yesu atakapokua [5] (wafilipi 3:13 – 14)

Kama tunajua Neno la Mungu, tunajua tunapoishi. Tunajua saa tunayoishi. Tunajua kilicho mbele yetu, tunaona tulikopita. Na kitabu cha Mungu ni ufunuo wa Yesu Krisot. Kazi zake katika nyakati zote ambayo ni ya kitabu cha Ufunuo na baadaye ahadi zake zinazokuja kwa hiyo ahadi zake zoe ni za kweli. Mungu hawezi akazungumza Neno bila kuthibitishwa. Kila Neno analolinena linaenda kutima [6]

Nukuu za Kiingereza

[1] Mtazame Yesu (kitabu cha 2 na 17) uk. 27

[2] Ile mbegu ya hitilafu Aya 21 – 25

[3] Mungu ndiye mtafsiri wake aya 9 – 18

[4] Edeni ya shetani uk. 5 – 6, 7

[5] Shalom (kitabu cha 13 na 5) Aya 137 – 143

[6] Mambo yatakavyokuwa Aya 26

Jiwe la kiroho la kujengea na. 151 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69 D-75328 Schomberge, Germany Simu (+49) 72357613 Fax (+49) 72353306

Anakuja mmoja na ukumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.

Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili andika kwa

Charles E. Y. Kanju,

Box 553 Korogwe - Tanga

E-mail: Chaelika@live1.com

Cellphone: 0784 704299/ 0718230098